

Hai Yetu



Jarida la Halmashauri

TOLEO MAALUMU, 2020

LINATOLEWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

Utekelezaji wa Ilani ya CCM 2015-2020 chini ya Serikali ya Awamu ya Tano Katika Wilaya ya Hai





Bodi ya Uhariri

Yohana Elia Sintoo

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Riziki Lesuya - Afisa Habari (W)

Herick Marisham - Afisa Mipango (W)

Msanifu Kurasa

Adrian Lyapembile - Afisa Habari

Mawasiliano

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Hai

S. L. P. 27

Hai - Kilimanjaro

Simu: 27-2974369

Fax: 27-2974368

Tovuti: www.haidc.go.tz

Barua pepe: ded@haidc.go.tz

Blogu: www.wilayayahai.blogspot.com

Karibu mpenzi msomaji wa Jarida la Hai Yetu, ikiwa ni Toleo Maalumu kwa ajili ya kuangazia Miaka Mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Rais kipenzi cha watu, mchapakazi wa mfano, jemedari John Pombe Magufuli.

Jarida hili litaangazia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi CCM pamoja na miradi mbalimbali iliyofanyika katika Wilaya ya Hai kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020 ikiwemo Miradi ya sekta za Afya, Elimu, Utawala, Maji.

Utekelezaji wa miradi hii ya maendeleo ni juhudi za serikali kuhakikisha kuwa wananchi wanasogezewa huduma muhimu katika maeneo yao ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hizo kutoka kwenye maeneo yao na kusababisha wananchi kupoteza muda wa kuzalisha mali.

Aidha jarida hili litaangazia mipango mbalimbali ya kuinua wananchi kiuchumi kwa kupitia Mpango wa Kunusuru kaya Masikini unaosimamiwa na TASAF, mpango wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake, vijana na vikundi vya watu wenye ulemavu ambao kwa maelekezo ya serikali kila halmashauri hutenga asilimia kumi 10% ya mapato yake ya ndani ili kutoa mikopo kwa makundi hayo ili kusaidia juhudi za kuwaongezea wananchi kipato kwa kufanya uzalishaji.

Jarida hili litakupitisha kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Hai kuangazia yale yote yaliyofanyika hususani yale yanayogusa maisha ya mwananchi kwenye kata 17 za wilaya hiyo.

Yohana Elia Sintoo

Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Hai

Wilaya ya Hai ni moja kati ya wilaya 6 za Mkoa wa Kilimanjaro.

Wilaya hii ilitengwa kutoka Wilaya ya Moshi mwaka 1975, ikipakana na wilaya ya Moshi kwa upande wa Mashariki, Arumeru na Siha upande wa Magharibi, Simanjiro upande wa Kusini, Rombo na hifadhi ya Mlima Kilimanjaro upande wa Kaskazini.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 Wilaya ya Hai ina jumla ya wakazi 210,533 kati yao wanawake 108,076 na wanaume 102,457 huku kasi ya ongezeko la watu ni asilimia 1.9 kwa mwaka, hivyo maoteo kwa mwaka 2020 ni watu 251,838 ambapo kati yao wanawake ni 128,747 na wanaume 123,091.

Wilaya ya Hai ina eneo la ukubwa wa Hekta 101,100 ambapo hekta 46,506 zinafaa kwa kilimo, hekta 27,297 zinafaa kwa mifugo, hekta 14,154 ni misitu na hekta 13,143 ni miamba. Shughuli za kiuchumi ni pamoja na biashara, Kilimo, Utalii, Ufugaji huku Kilimo kikichukua 80% ya shughuli za wakazi wote wa Wilaya.

Katika Wilaya ya Hai kuna kanda 4 zenye tabianchi tofauti kwa sababu iko kwenye mteremko wa Mlima Kilimanjaro

Kanda ya Kilele cha Mlima iko juu ya kimo cha mita 1,800 Usawa wa Bahari pamoja na kilele cha Kibo ikiundwa zaidi na maeneo ya mbuga na hifadhi ya Taifa hivyo hakuna wakazi wa kudumu ikichukua asilimia 27 za eneo la wilaya. Kanda ya Juu iko kwenye kimo kati ya mita 1,666 na 1,800 juu ya Usawa wa Bahari ambayo inafaa kwa kilimo cha kahawa na ndizi. Wananchi walio wengi ni wakulima wadogo wanaofuga ng'ombe wa maziwa na kuuza maziwa.

Kanda ya Kati ipo kwenye kimo kati ya mita 900 hadi 1,666 juu ya Usawa wa Bahari ikiwa inapokea mvua kati ya milimita 700 hadi 1250 kwa mwaka ikifanana na kanda ya juu kwa shughuli za kilimo na ufugaji.

Kanda ya Chini iko kwenye kimo chini ya mita 900 juu ya Usawa wa Bahari ambapo mvua inapungua hadi milimita 500-700 kwa mwaka. Mazao yanayostawi ni pamoja na maharagwe, mahindi, alizeti na mpunga. Ufugaji wa ng'ombe wa kienyeji, mbuzi na kondoo unafanyika kwenye ukanda huu.

Bilioni 3 Zaimarisha Huduma ya Maji Wilayani Hai



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli akizinda moja ya miradi iliyotekelezwa na serikali katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo wa utawala wake.

“Maji ni uhai” ni moja ya msemmo maarufu kwa wananchi wengi nchini Tanzania; msemmo huu unafahamika na watu wa rika zote na unathibitishwa na wataalamu wa afya hasa pale wanapoelezea kuwa mwili wa mwanadamu unaundwa kwa asilimia 70% na maji.

Matumizi ya maji kwa mwanadamu yanaanza kwenye kunywa, kupikia, kuoga, kuosha na matumizi mengine kiasi cha kufanya bidhaa muhimu kwenye maisha ya mwanadamu na kwamba siku ya mwanadamu haiwezi kupita bila kutumia bidhaa hii muhimu.

Katika kufahamu umuhimu wa maji kwene jamii; serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuimarisha miradi mbalimbali ya maji ili kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa mahitaji yao ya nyumbani na

kwenye shughuli zao za kila siku.

Ilani ya Uchaguzi ya chama kinachoongoza Serikali Chama cha Mapinduzi Ibara ya 54 (iii) inazungumzia Kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo ya miradi ya Kitaifa kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 90 mwaka 2020.

Akizungumzia sekta ya maji wakati wa hotuba yake ya kufunga mkutano wa 19 wa Bunge; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli amesema jumla ya miradi ya maji 1,423 kati yao miradi 1,268 ni ya vijijini na miradi 155 ni ya mjini na kuongeza upatikanaji wa maji vijijini kwa 47% mwaka 2015 hadi 70.1% mwaka 2020 na mijini kutoka 74% mwaka 2015 hadi kufikia 84% mwaka 2020.

Wilaya ya Hai ni moja ya maeneo yanayonufaika na utekelezaji wa kifungu hicho cha ilani ya uchaguzi kwa kutekelezwa miradi kadhaa ya maji ikiwemo upanuzi wa skimu ya Losaa-Kia iliyogharimu shilingi 2,764,314,975.00 ambayo inahudumia vituo 34 katika vijiji vya Sanya station, Tindigani, Mtakuja na Chemka ambapo hadi sasa huduma ya maji inapatikana katika vituo vyote na wakazi wapatao 19,729 wanapata huduma ya maji.

Mradi wa skimu ya maji ya Lya-mungo-Umbwe unaohudumia kata za Narumu, Masama Kusini, Mnadani, Machame Mashariki na Weruweru umefanyiwa ukarabati wa miundombinu ili kufanikisha jukumu la usambazaji maji kwa gharama ya shilingi 65,399,435.00. Mpango wa ‘Lipa kwa Matokeo’ (Payment by Results) umesaidia wilaya ya Hai kupata kiasi cha shilingi 515,075,227.44 zilizosaidia kufanya ujenzi mpya wa miundombinu ya bomba na kuongeza vituo vipya 34vya kuchotea maji ambavyo vina uwezo wa kuhudumia wakazi wapatao 8,500. Vilula 19 vimekamilika na vimeanza kutumika huku kazi ya kukamilisha vilula vingine 15 bado inaendelea. Mpango huo umefanyika kwenye kata za Masama Kusini na Bomang’ombe ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa na ongezeko la wakazi.

Wilaya ya Hai inaendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa kutegemea vyanzo vya maji vina-vyopatikana ndani ya wilaya hiyo.

Serikali Yakabidhi Ardhi kwa Mjane Aliyedhulumiwa



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli akitoa maelekezi ya kazi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Ndg. Yohana Sintoo katika eneo la Bomang'ombe wilayani Hai.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli ameagiza kupatiwa eneo la ardhi Bibi Hawa Shila mkazi wa Kijiji cha Kimashuku Kata ya Mnadani wilayani Hai ili apate eneo la makazi na kufanya shughuli za kilimo.

Akitoa maelekezo ya Rais kwenye mkutano wa Kijiji hicho; Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya amesema kuwa Bibi Shila alimwandikia barua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuomba usaidizi wa kuzuia kuhamishwa eneo ambalo ameishi kwa zaidi ya miaka 40 au kupatiwa eneo jingine la makazi na kilimo ili aweze kujikimu na kuendesha maisha yake.

“Mheshimiwa Rais ameona barua yako na amenielekeza kuhakikisha kuwa unapata haki yako. Leo nimekuletea barua ya kukupa eneo la kufanya shughuli za kilimo na eneo la makazi” Amesema

Sabaya.

Bibi Hawa Shila alifikia uamuzi wa kumwandikia barua Rais magufuli baada ya kuhamishwa kwenye eneo la mnadani lililopo Kata ya Mnadani wilayani Hai ambapo ameishi kwa zaidi ya miaka 40 huku akidaiwa kuishi eneo hilo kinyume na taratibu.

“Walini fukuza nikawauliza sasa wanangu niende wapi wakase-

ma sijui mama, eneo hilo nimezika mume wangu na mdogo wangu hapohapo; nimezalia watoto wangu hapohapo na nimepata wajukuu hapo, basi wakaanza kunipiga vita sasa.”

Bibi Shila amemshukuru Mkuu wa wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya kwa kumsaidia kupata eneo hilo na zaidi akimwomba baraka na maisha marefu Rais John Magufuli aliyemwita mtetezi wa wanyonge.

Baada ya maelekezo hayo Sabaya amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Yohana Sintoo akishirikiana na Afisa Ardhi wilaya kusimamia umiliki wa eneo la Bibi Shila kwa kumpatia ofa na hati pamoja na kutengeneza ramani na miundombinu inayohitajika kwa kuzingatia mipaka ya eneo hilo. Eneo la ekari moja ambalo amekabidhiwa Bibi Shila linatokana na ekari tisa zilizokuwa za serikali zilizopo Kijiji cha Kimashuku Kata ya Mnadani ambazo zimegawiwa kwa kijiji hicho mwezi June 2020 kwa ajili ya kujenga soko, zahanati na kufanya shughuli za maendeleo.



Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya akizungumza na wana-nchi wa Kijiji cha Kimashuku kutatua mgogoro wa ardhi akiambatana na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Hai Wang'uba Maganda, Katibu Tawala Upendo Wella, Mkurugenzi Yohana Sintoo na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

Makamu wa Rais Azindua Wodi ya Wanawake



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan akiwa hutubia wananchi wa Wilaya ya Hai mara baada ya kuzindua jengo la Wodi ya Wanawake katika hospitali ya wilaya hiyo

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya ziara ya kikazi katika wilaya ya Hai na kuzindua jengo la wodi ya wanawake katika hospitali ya wilaya hiyo ikiwa ni utekelezaji wa kazi za Serikali unaofanywa na serikali ya wamu ya Tano chini ya Dr John Pombe Magufuli.

Akizindua wodi hiyo ambayo imejengwa kwa fedha mapato ya ndani ya halmashauri kwa kutumia fedha zinazokusanywa na hospitali hiyo kupitia mpango wa Bima ya Afya Makamu wa Rais amepongeza juhudi za halmashauri hiyo ujenzi wa wodi na kusema ni jambo la mfano na linafaa kuigwa na halmashauri nyingine.

Makamu wa Rais pia amewasihi wahudumu wa afya katika hospitali hiyo na nyinginezo kuifanya kazi hiyo kwa uaminifu na uadilifu ili kujipatia thawabu kwa Mungu.

Amesema kuwa kutakuwa hakuna maana ya kuwa na miundombinu mizuri kama wodi na mengine wakati watoa huduma wasiposimamia kufanya kazi yao kwa weledi na kuwajali wagonjwa wanaopatiwa huduma.

Katika hatua nyingine Makamu wa Raisi amehutubia mamia ya wananchi waliokusanyika katika eneo la Ofisi ya Kijiji cha Kwasadala huku akisifu jitihada zinazofanywa na halmashauri kupitia Mkuu wa Wilaya hiyo Lengai Ole Sabaya

ambapo amesema kuwa kiwango cha ukusanyaji wa mapato kimeongezeka kwa zaidi ya 200%.

Aidha Makamu wa Rais amekelea tabia ya baadhi ya viongozi wanaosababisha migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na vyama vya ushirika na kuagiza mamlaka husika kushughulikia na kutatua migogoro hiyo.

Makamu wa Rais amehitimisha ziara yake ya kikazi mkoani Kilimanjaro ambapo alitembelea wilaya za mkoa huo akiwa ameambatana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mhe. William Lukuvi pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mhe. Selemani Jaffo.



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan akimfariji mmoja wa wagonjwa aliowakuta wakipata huduma kwenye Hospitali ya Wilaya ya Hai kabla ya kufanya uzinduzi rasmi wa huduma katika jengo hilo



Muonekano wa ndani wa wodi ya wanawake katika Hospitali ya Wilaya ya Hai ambalo limeanza kutumika baada ya kuzinduliwa na Makamu wa Rais



Jengo la Wodi ya Wanawake katika Hospitali ya Wilaya ya Hai ambalo limeanza kutumika baada ya kukamilisha ujenzi wake na kupunguza adha ya wagonjwa kutumia jengo moja lililotenganishwa wanaume na wanawake na kufanya hospitali kuwa na wodi tofauti za wanawake na wanaume



Ujenzi wa jengo la Duka la Dawa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Hai imesaidia kuimarisha upatikanaji wa dawa saa 24 kila siku za wiki kwa wagonjwa wote wa hospitali ya wilaya na wanaotibiwa kwenye vituo vingine vya kutolea huduma za afya

Serikali Inatambua Mchango wa Sekta Binafsi



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa akiwahutubia wananchi wa Wilaya ya Hai kwenye ziara yake ya kikazi ya siku moja katika wilaya hiyo

Serikali imesema inatambua jitihada zinazofanywa na taasisi za dini pamoja na mashirika binafsi katika kuchangia masuala ya elimu hapa nchini. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Shule ya Sekondari Jumui-

shi ya Mtakatifu Pamachus iliyojengwa na Kanisa Katholiki; Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa amesema kuwa jitihada za kuwekeza katika elimu zinazo-

fanywa na mashirika ya dini pamoja na taasisi binafsi ni mchango tosha wa kusaidia elimu hasa katika kuyapa kipaumbele makundi maalumu.

Wakati wa uzinduzi wa shule hiyo Waziri Mkuu amesema kuwa Serikali itatoa kiasi cha shilingi million kumi kusaidia kuendeleza miundombinu ya shule hiyo.

Amesema serikali imeboresha sekta ya elimu na tayari kwa sasa mazingira ya

elimu yamezidi kuboreshwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule za msingi elfu kumi na saba, shule za sekondari pamoja na ujenzi unaoendelea katika chuo cha ualimu Patandi cha jijini Arusha.

Waziri Mkuu amemwagiza Mkurugenzi wa halmashauri ya Wilaya ya Hai kutembelea shule zinazomilikiwa na taasisi za dini na binafsi ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo na kushauri namna bora ya kuzitatua. Aidha ameiagiza idara ya ukaguzi wa elimu kupitia na kukagua shule zote ili kuona kama zinakidhi vigenzo ikiwa ni pamoja na kuwa na mitaala sahihi inayotakiwa kutumika.

Naye Askofu wa Jimbo Kuu Katholiki Arusha Muhashamu Baba Askofu Isack Aman amesema kuwa kanisa liliona kuna hitaji la msingi la kujenga shule zenye kupokea wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuhakikisha kunakuwepo na fursa sawa kwa wote.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akiweka jiwe la msingi kuashiria uzinduzi wa Shule ya Sekondari Mchanganyika ya Pamachus

Mifumo ya Kielektroniki Yaiboresha Wilaya ya Hai



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Selemani Jafo aki-kagua ujenzi wa miundombinu ikiwemo mifumo ya kielektroniki kwenye Hospitali ya Wilaya ya Hai

Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yamepelekea mabadiliko makubwa kwenye maisha ya mwanadamu hasa katika karne hii ya 21 inayotambuliwa kama karne ya Teknolojia. Tanzania ikiwa sehemu ya Dunia inakutana na matokeo ya mabadiliko ya teknolojia yanayosaidia kuimarisha utendaji wa kazi mbalimbali ikiwemo maboresho katika mawasiliano, utunzaji wa kumbukumbu, Uwazi na utawala bora pamoja na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utekelezaji wa kazi za serikali na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Wilaya ya Hai kwa kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) chini ya

usimamizi wa waziri wa wizara hiyo Selemani Jafo imefaidika na maendeleo ya Teknolojia hasa baada ya serikali kuanza kutumia mifumo ya kielektroniki kusimamia utoaji wa huduma mbalimbali za serikali katika wilaya hiyo ambapo Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Anold Malisa anaelezea baadhi ya mifumo inayotumika katika Halmashauri hiyo.

Mfumo unaosimamia utoaji huduma kwenye vituo vya kutolea huduma za afya (GoT-HOMIS) ni mfumo wa kielektroniki unaosimamia shughuli nzima za kutoa huduma za afya kwa kuratibu mwenendo wa mgonjwa tangu anapofika kuandikishwa Hospitali, kukutana

na daktari, kupata vipimo maabara hadi anapopatiwa dawa.

Mfumo huo umesaidia kuimarisha utunzaji na upatikanaji wa kumbukumbu, utoaji wa taarifa za dawa, fedha, watumishi n.k, kuzuia mianya ya upotevu wa mapato yanayopatikana kwa tozo mbalimbali za uchangiaji huduma za afya pamoja na kurahisisha zoezi la ufuatiliaji wa taarifa za mgonjwa.

Mfumo mwingine unaotumika katika Wilaya ya Hai ni mfumo wa mapato (LGRCIS) ambao unasimamia zoezi la kukusanya maduhuli ya serikali kielektroniki kwa kutumia mashine za mauzo au POS ambazo zinapatikana kwenye kila eneo la kukusanyia ushuru wa Halmashauri huku kila pesa inayokusanywa inatolewa risiti na kiasi hicho kuonekana kwenye mfumo mkuu hivyo kuondoa mianya ya upotevu wa mapato.

Mfumo wa malipo ya serikali (GEPG) ni moja ya mafanikio makubwa katika kuimarisha ukusanyaji wa maduuli ya serikali kwani malipo yote yanafanyika kwa namba ya ankara (control number) inayomwezesha mlipaji kuwasilisha malipo yake kupitia benki au mitandao ya simu kutoka mahali popote duniani.

Inaendelea uk.7



Afisa Ustawi wa Jamii akimhudumia mteja wake kwa kutumia mfumo kielektroniki wa kutolea huduma za afya.

Mifumo ya Kielektroniki Inatoka uk.6

kwa namba ya ankara (control number) inayomwezesha mlipaji kuwasilisha malipo yake kupitia benki au mitandao ya simu kutoka mahali popote duniani.

Planrep ni mfumo wa mipango ya bajeti na kutoa taarifa za fedha inayotoa nafasi kwa kila idara na vitengo ndani ya halmashauri kufanya maandalizi ya mipango yao ya kifedha kielektroniki ikiwa ni msaada mkubwa kupunguza matumizi ya kusafiri kuwasilisha bajeti kwani mfumo unauunganisha ngazi ya Vituo, Wilaya, mkoa

hadi ngazi ya Wizara na Kitaifa. Mfumo huu umesaidia sana kurahisisha maandalizi na utekelezaji wa masuala ya kibajeti na fedha.

Mfumo wa matumizi umegawanyika katika sehemu mbili kukiwa na mfumo wa matumizi ngazi ya halmashauri (EPICOR) na mfumo wa matumizi ngazi ya vituo vya kutolea huduma (FFARS) unaotumika kwenye vituo vya huduma za afya na shule zote za serikali ambao matumizi yake yamesaidia kudhibiti upotevu wa fedha, kuthibiti matumizi holela ya fedha ikiwemo fedha mbichi

pamoja na kuimarisha upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha kwenye halmashauri pamoja na vituo vya huduma.

Pamoja na mifumo hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Hai inafaidika kwa kutumia mifumo mbalimbali ya kielektroniki katika sekta za Afya, Elimu sekondari na Elimu msingi, mifumo ya upashanaji habari ikiwemo barua pepe zenye kikoa cha Kitanzania (.tz), tovuti za serikali zenye kubeba taarifa za mambo mbalimbali yanayofanyika kwenye halmashauri



(www.haidc.go.tz). Matumizi ya TEHAMA kwenye utekelezaji wa kazi za Serikali katika Wilaya ya Hai ni kichocheo chanya katika kuleta maendeleo ya jamii ya watu wa Hai kwa ujumla wao lakini pia inagusa maendeleo ya mtu mmojammoja na hatimaye kuwafanya watu wote waweze kupata huduma stahiki kwa haraka zaidi.



Watumishi wa Idara ya Afya kwenye Hospitali ya Wilaya ya Hai wakiwahudumia wananchi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki. Kushoto ni Daktari akimhudumia mgonjwa na kulia ni mfamasia akimpatia dawa mgonjwa kwa kutumia mfumo wa kutolea huduma za afya GOTHOMIS.

Waziri Lukuvi Atoa Suluhisho Mgogoro wa Ardhi Lambo Estate

“Tunaishukuru sana serikali kwa hatua hii, ni kitu ambacho hatu-kutegemea kwani tangu mwaka 1996 mimi mwenyewe nafuatilia suala hili na hatukuwahi kupata su-luhu, namshukuru sana Rais John Pombe Magufuli pamoja na serikali yote”

Hii ni kauli ya Saidi Omari ambaye ni miongoni mwa wananchi walio-hudhuria kikao kati ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi na wananchi wa kijiji cha Nshara pamoja na bodi ya mradi wa umoja wa vyama vitatu vya ushirika vya Foo, Nronga na Wari katika shamba la Lambo Estate.

Katika kikao hicho Waziri Lukuvi ameagiza kaya 78 za wananchi waliokuwa wafanyakazi wa mashamba ya mkongwe (Lambo Estate) wilayani Hai Mkoani Kilimanjaro kupe-wa ekari 156 ikiwa ni utatuzi wa mgogoro kati ya wananchi hao na mradi wa umoja wa vyama hivyo.

Agizo hilo limekuja baada ya mgogoro wa shamba la hilo na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Nshara ulioanza tangu miaka ya tisi-ni baada ya wananchi hao kutuma maombi serikalini wakiomba kupewa eneo la makazi ikifuatiwa na tukio la ajira yao kukoma ambapo mwaka 2001 wafanyakazi hao wali-fungua kesi kwa kutoridhika na stahiki walizolipwa na mradi huo.

Mwaka 2003 Mahakama iliamuru wafanyakazi hao waendeleo kuisi kwenye nyumba za ushirika na wapewe hekari 50 kwa ajili ya ku-wawezesha kufanya shughuli za kili-mo pasipo kujenga makazi ya kudu-mu.

Akizungumza na wananchi pamo-



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi William Lukuvi akizungumza na waliokuwa wafanyakazi wa Lambo Estate kutatu mgogoro wa ardhi.

ja menejimenti ya bodi ya vyama hivyo Waziri Lukuvi amesema serikali ya Awamu ya Tano haiwezi kuona wanyonge wakiendelea kuteseka kwa sababu ya watu wachache na kwa sababu hiyo ameagiza wananchi hao wasifukuzwe katika eneo hilo.

“Hamuwezi kujikusanya huko wajanja wachache na kutaifisha ardhi za vijiji alafu mnawakodisha wananchi ardhi na kutumia fedha hizo, huu ni ukoloni kabisa safari hii tutanyoosha maneno yote haya yaliyopinda kwani serikali hii ya awamu ya tano haitacha mambo haya yapite hivi” amesisitiza Lukuvi.

Kufuatia hatua hiyo amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya kusimamia zoezi la upimaji wa ardhi hiyo ili kuziwezesha kaya hizo kupata hekari 2 kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo na uzalishaji wa chakula kwa masharti ya kutouza maeneo watakayopewa. Katika hatua nyingine Waziri Lukuvi ameagiza uongozi wa NDC kulipa kabla ya mwezi Disemba kodi ya ardhi ya eneo wanaolimiki na kufanyia kazi tangu walipokabidhiwa eneo hilo ili kuwawezesha kupewa hati miliki ya eneo hilo na

endapo hawataweza kufanya hivyo taratibu za kulirudisha eneo hilo kwa serikali zitachukuliwa.

Akizungumza katika eneo hilo la machine tools, Mhe. Lukuvi ameagiza wananchi wote waliomilikishwa maeneo katika eneo hilo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 1000 na wameshindwa kuliendeleza wapewe notisi ya siku tisini ili taratibu za kuchukua eneo hilo na kwa wale waliopimiwa na hawana hati ya umiliki orodha yake ifikishwe kwake na wapewe taarifa ya kuto-kuwa na umiliki wa eneo hilo.

“Asiye na hati niorodhesheni tu nitatoa idhini ili tutangaze watanzania wengine na wawekezaji wageni wenye uwezo wa kuwekeza waje wawekeze, eneo hili limekaa muda mrefu pasipo kuendelezwa na lipo mjini”

Naye Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya amemweleza Waziri kuwa amepokea maagizo yote yaliyotolewa kwenye ziara hiyo na kuweka bayana kuwa atayatekeleza kwa nguvu zote ili haki ya kila mhusika ipatikane lakini pia kuiwezesha serikali kukusanya mapato stahiki kutokana na kodi zitakazolipwa kwenye maeneo hayo.

TAMISEMI Yapongeza Juhudi Kuboresha Maisha Wilayani Hai

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Mwita Waitara amewataka watumishi na viongozi katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuimarisha maendeleo ya wananchi kama inavyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi inayosimamia serikali. Akizungumza kwenye mkutano na watumishi wa wilaya hiyo, Naibu Waziri Waitara amesema kuwa Wizara ya TAMISEMI inaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na viongozi hususan Mkuu wa Wilaya hiyo Lengai Ole Sabaya zikiwa na juhudi za kuboresha maisha ya wakazi wa wilaya.

“Endeleeni kutafuta haki za wananchi waliodhulumiwa; wale walioguswa wakija kwetu tutaangalia kama mmewaonea, lakini kama mmesimamia haki sisi kama TAMISEMI tutawaunga mkono”. Amesema.

Aidha amewashauri viongozi na watumishi kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria na taratibu husika bila kupendelea wala kumuonea mtu yeyote. Awali akitoa tathmini ya



Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Mwita Waitara

kazi, Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya amemweleza Naibu Waziri wa TAMISEMI kuwa wilaya inaendelea kutatua changamoto za wananchi kwenye masuala ya ardhi, ushirika na aina nyingine za madhila ikiwemo kuondoa matabaka miongoni mwa wananchi.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Hai Dkt. Irene Haule amesema kwa kushirikiana na vyama vya ushirika wilaya imeanza ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kijiji cha Longoi kitakachohudumia wakazi wa kata za Masama Rundugai, Weruweru na Mnadani zenye Zaidi ya wakazi 30,000 kikitoa huduma zote za kawaida na dharura.

Kwa nyakati tofauti baadhi ya wananchi wameonesha kufu-

rahia wazo la kupata kituo cha afya kwenye maeneo yao ambacho kitawapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kupata huduma huku waki-ahidi kuwa tayari kushirikiana na serikali kwa kuchangia nguvukazi ili kukamilisha ujenzi wa kituo hicho.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mwita Waitara amefanya ziara ya kikazi ya siku moja kwenye wilaya ya Hai ambapo amepata wasaa wa kuzungumza na watumishi wa Wilaya hiyo wakiwemo wakuu wa shule za sekondari, waratibu wa elimu ngazi ya kata, watendaji wa vijiji na kata pamoja na wakuu wa idara na vitengo pamoja na watumishi wa makao makuu ya halmashauri.

Migogoro ya Wakulima Wafugaji Kupatiwa Ufumbuzi

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Elisante Ole Gabriel ameitaka jamii ya wafugaji kufuga kibiashara kwa kuwa na mifugo michache yenye afya nzuri na kutii sheria za nchi ili kuzua migogoro baina yao na wakulima. Amesema serikali ya awamu ya tano inawathamini na kuwapenda wafugaji kwa kuwa wana haki sawa na wakulima na wafanyakazi hivyo nao wanao wajibu wa kutii mamlaka na sheria zilizopo.

Amesema wizara yake inatekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambapo ibara ya 25 kifungu a hadi q inawazungumzia wafugaji na kuwaondoa hofu iliyopo miongoni mwao ya kwamba serikali haiwathamini.

“Mhe. Waziri Mpina amenituma niwaambie na niwahakikishie wananchi wa Hai hasa wafugaji kuwa Rais John Magufuli ni kipenzi cha wafugaji, hivyo amewataka mmtunzie heshima hiyo na mjue kuwa serikali inatambua haki ya wafugaji na mtembee kifua mbele” amesema Prof. Gabriel.

Amesema kuwa mifugo haiwezi kuendelezwa bila ya kuwaendeleza wafugaji kwa kua vyote vinategemeana na kwamba wizara inaendelea kuboresha na kufanyia kazi changamoto za wafugaji kwa kuwa mifugo inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi akitolea mfano wa ng’ombe na mazao yake ambayo imeajiri kundi kubwa la wananchi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya amewaagiza wenyeviti wa vitongoji, vijiji na watendaji wa vijiji na kata kutopokea fedha zozote zinazotokana na migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika maeneo yao badala yake watoe taarifa ya migogoro hiyo kwa Mkurugen-



zi Mtendaji na ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Sanya Station kata ya Kia Wilayani Hai, Sabaya amesema serikali haiwezi kuvumilia kuona migogoro hiyo ikien-delea na kuwaasa watendaji na wenyeviti kuepuka kuwa sehemu ya mgogoro kutasaidia kwa kiasi kikubwa kumaliza migogoro hiyo.

“Kwa namna yoyote ile serikali haitavumilia unyanyasaji wowote utakaofanywa kwa wafugaji wala haitavumilia kuona wafugaji wanaonea wakulima, hivyo ni marufuku kwa wafugaji kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kila mkulima abaki katika eneo lake ili kuepuka migogoro.” Alisisitiza Sabaya.

Naye Katibu wa wafugaji nchini Magembe Mkaoye ameiomba serikali kuweka

mpango wa matumizi bora ili kutenga eneo la kulishia mifugo na eneo la wakulima ili kupunguza migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Ameongeza kuwa wafugaji wanategemea mifugo katika kukidhi mahitaji yao ya kifamilia pamoja na uchumi wao hivyo ameasa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji kuheshimiwa ili kuepuka changamoto ambazo zin-aarudisha nyuma maendeleo.

Kwa upande wao wananchi waliopata nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya wenzao wameiomba serikali kuwatengea maeneo rasmi ya malisho na kuwajengea majosho ya mifugo na kuwapa elimu ya kuhudumia mifugo na kutambua magonjwa yanayowasumbua, maombi ambayo Katibu Mkuu aliahidi yatafany-iwa kazi mapema.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Elisante Ole Gabriel amefanya ziara ya kikazi ya siku moja katika Wilaya ya Hai akiwa na lengo kuu la kufahamu changamoto zinazowakabili wafugaji ikiwa ni hatua ya kuimarisha shughuli za ufugaji nchini.

Serikali Yajivunia Mafanikio Sekta ya Madini



Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbas akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Ndg. Yohana Sintoo alipotembelea halmashauri hiyo.

Serikali inajivunia mafanikio yanayotokana na mageuzi katika sekta ya madini yaliyopatikana ndani ya miaka mitatu ya mwanzo ya serikali ya awamu ya Tano inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuli.

Akizungumza na wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro na maeneo jirani kupitia kituo cha redio Boma Hai siku ya Jumapili 09/12/2018 Msemaji Mkuu wa Serikali amesema kuwa serikali imefanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya madini.

Dkt. Abbas amebainisha kuwa sekta nzima ya madini nchini imeongeza makusanyo kutoka chini ya shilingi Biliioni 190 na hadi kufikia mwezi Julai 2018 mapato yamefikia shilingi billioni 301 ikiwa ni ishara ya kuongezeka kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali ambayo ndiyo yanatumika kuwapatia wananchi huduma za elimu bila malipo pamoja na maboresho kwenye

huduma mbalimbali. Akilinganisha hali ilivyokuwa kabla ya marekebisho yaliyofanyika, Dkt. Abbas anasema kuwa mapato ya serikali kutokana na madini yalikuwa kati ya shilingi milioni 71 – 74 kwa mwaka, kwenye machimbo ya Tanzanite ambayo miezi 8 baada ya kujengwa ukuta unaodhibiti utoroshaji wa madini na kuongeza uwazi katika upatikanaji wa mapato ya serikali.

“Mererani wamepelewa lengo la kukusanya shilingi billion 1.5 ambayo kwa muda wa miezi 5 hadi kufikia mwezi Novemba tayari wamefanikiwa kukusanya shilingi milioni 800 ikiwa ni zaidi ya nusu ya lengo.” Amesisitiza Dkt. Abbas. Kwa upande wa dhahabu ya mkoani Geita, nchi ilikuwa inapoteza mapato kwenye kusafisha dhahabu ambapo mwanzo shughuli hizo zilifanyika

Mwanza na hakuna aliyejua kilichopatikana.

“Serikali iliagiza kuwa mashine zote za kusafisha dhahabu ziwekwe ndani ya mkoa husika na hadi sasa zipo mashine zaidi ya 20 zinazosafisha dhahabu kukiwa na uangalizi wa maafisa wa serikali na kufanikiwa kuongeza dhahabu kutoka kilo 70 – 160 kwa mwezi na kuongeza mapato ya serikali kwenye dhahabu kutoka milioni 400 kwa mwezi hadi zaidi ya shilingi million 900.” Ameongeza.

Aidha, Dkt. Abbas amewataka wananchi kuendelea kuiamini serikali yao na kuingua mkono hasa wakati huu wa kutekeleza miradi mikubwa itakayobadilisha kwa kiasi kikubwa maisha ya jamii nzima ya Tanzania kwani kwa kuongeza mapato ya serikali kunaipa nguvu katika kutoa huduma bora kwa wananchi wake.

Akizungumzia maendeleo ya kufikia uchumi wa kati kwa kuwa na viwanda, Dkt. Abbas amesema kuwa hadi sasa matokeo chanya yanazidi kuonekana kwani wapo wanaonufaika na viwanda kwa kupata ajira moja kwa moja lakini pia wapo wale wanaonufaika kwa uwepo wa viwanda kwenye maeneo yao.

“Takribani watanzania 26,000 wameajiriwa moja kwa moja kwenye viwanda na zaidi ya wananchi 100,000 wameweza kuanzisha biashara na kujiajiri kwa sababu ya viwanda vilivyopo” Ameongeza.



Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Hassan Abbas na Mwenyekiti wa Chama cha Maafisa Habari wa Serikali (TAGCO) Paschal Shelutete wakizungumza na wananchi wa Wilaya ya Hai na mikoa ya Kanda ya Kaskazini kupitia kituo cha Redio Boma Hai kinachomilikiwa na Halmashauri ya wilaya ya Hai

Halmashauri ya Hai Yashauriwa Kuongeza Mikopo Wajasiriamali

Wito umetolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kutoa kiwango kikubwa cha fedha wanazowapa wanawake, vijana na wenye ulemavu ili kuwawezesha kutekeleza miradi yenye tija kwa jamii husika.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Taifa wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Comrade Kheri James kwenye mkutano wa ndani na wanachama wa chama hicho uliofanyika katika ukumbi wa Filomena wilayani Hai.

Amesema mikopo hiyo iangalie uwezekano wa wanaokopeshwa kuzalisha ajira za watu wengine ili ku-saidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira lakini pia kuwzesha wakopaji kutengeneza kipato cha kaya zao. Aidha James ametumia mkutano huo kuwakumbusha vijana na wanachama wote wa Chama cha Mapin-



Mwenyekiti wa UVCCM Taifa Kheri James akiwasilimi wananchi wa Wilaya ya Hai akiwa na Mkuu wa Wilaya ya hiyo Lengai Ole Sabaya

bu wa kutekeleza kwa chama na Taifa kwa ujumla hasa katika kipindi hiki ambapo nchi inapitia mabadiliko makubwa kwenye sekta zote kuelekea maendeleo endelevu. “Leo hapa Hai nataka niwakumbushe umuhimu wa kuilinda nchi yetu, kuipenda nchi yetu na kuithamini nchi yetu. Nchi

yetu ilipokuwa, ilipo na inapoelekea; kila mmoja anajua uelekeo wa nchi hii.” “Ukishakuwa na miundombinu ya uhakika kwa anga, miundombinu ya uhakika kwa maji, miundombinu ya barabara; uchumi wetu utakuwa wapi baada ya leo” Amewataka vijana kujiandaa kushiriki kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika miezi michache ijao kwa kupiga kura na kupigiwa kura kwa wale wataogomba nafasi mbalimbali.

Kwa upande mwingine Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya ame-

wakumbushwa wana-chama kuwa hakuna kiongozi mwenye mgombea katika kinyang’anyiro cha kuwania uteuzi wa CCM kwa nafasi ya ubunge wa jimbo la Hai. Nao Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro Ivan Moshi na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Hai Cedrick Pangani wamemwaki-kishia Mwenyekiti wa UVCCM Taifa kuwa wataendelea kushirikiana na vijana na makundi mengine kwenye jamii kuhakikisha kuwa chama chao kinapata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi mkuu ujao.



Mwenyekiti wa UVCCM Taifa Kheri James akiwasili kwenye eneo la mkutano akipokelewa na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Hai Cedrick Pangani na viongozi wengine wa chama wa Mkoa wa Kilimanjaro

Kamati ya Siasa CCM Mkoa Kilimanjaro Yaridhishwa Utekelezaji Miradi Hai



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Ndg. Yohana Sintoo akitoa maelezo ya ujenzi wa maabara shule ya sekondari Tambarare katika wilaya hiyo mbele ya kamati ya siasa ya CCM Mkoa wa Kilimanjaro

KAMATI ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kilimanjaro imesema kuwa imeridhika na hali ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo inayotekelezwa na halmashauri ya Wilaya ya Hai

Kauli hiyo inatolewa na Mwenyekiti wa CCM, Mkoani Kilimanjaro, Patrick Boisafi baada ya kutembelea miradi sita ya kimaendeleo ikiwemo ya elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Boisafi amesema kuwa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015 /2020 katika wilaya ya Hai umelekezwa kwa kuzingatia ubora na viwango vinavyostahili kutokana na ushirikiano na usimamizi mzuri wa wataalamu pamoja na viongozi wa Chama hicho ngazi ya wilaya.

Akiwa katika mradi wa shule ya Sekondari ya Tambarare iliyoanza kupokea wanafunzi mwaka huu amesema kuwa uanzishwaji wa shule hiyo umesaidia kuboresha elimu kwa wanafunzi wanaofaulu kuingia kidato cha kwanza ambao walikuwa wanatembea umbali wa kilometa 24 kwenda na kurudi hadi shule ya sekondari ya KIA

Mwenyekiti huyo amesema kupatikana kwa usajili wa shule hiyo kutapunguza adha ya watoto wa vijiji vya Mtakuja na Tindigani kutembea mwendo mrefu kufuata elimu na pia uanzishwaji huo utasaidia kupunguza tatizo la mimba za utotoni kwa wanafunzi

wa maeneo hayo.

Boisafi amesema kuwa halmashauri imeweza kutoa fedha za makusanyo ya ndani kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo ni agizo la serikali la kila halmashauri kutenga fedha za mikopo asilimia 10 ya makusanyo halisi ya ndani.

Aidha ameipongeza halmashauri kwa kutekeleza ilani kwa kutoa mikopo ya fedha kiasi cha zaidi ya milioni 109 kwa vikundi 27 kati ya vikundi hivyo 18 ni wanawake, 6 ni vya vijana na vikundi vitatu vya watu wenye ulemavu vimenufaika na mkopo huo.

Hata hivyo, amewataka watumishi wa umma kuwa mstari wa mbele kuelezea miradi inayotekelezwa na serikali ya awamu ya tano chini ya Uongozi wa Rais na mwenyekiti wa CCM Taifa Dkt John Magufuli ili wananchi wengi wafahamu umuhimu wa juhudi za maendeleo zinazofanywa na serikali.



Muonekano wa Maabara kwenye Shule ya Sekondari Tambarare baada ya ujenzi kukamilika

Nyumba za Watumishi Zapunguza Adha kwa Walimu Wilaya ya Hai



Jengo la nyumba wa walimu Six in one shule ya Sekondari Sawe



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Ndugu Yohana Sintoo akitoa maelezo ya ujenzi wa nyumba wa walimu Six in one shule ya Sekondari Sawe kwa kamati ya siasa ya CCM Mkoa wa Kilimanjaro

Mafanikio katika utekelezaji wa majukumu huchangiwa na mambo mengi ikiwemo utayari wa watekelezaji, upatikanaji wa mahitaji muhimu, ushirikiano wa washiriki lakini pia mazingira rafiki ya utekelezaji wa majukumu husika.

Katika sekta ya elimu kuna mambo kadhaa ya msingi yanayotakiwa kuzingatiwa ili kufanikisha jukumu la kuelimisha wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu.

Wilaya ya Hai imetambua umuhimu wa kuimarisha mazingira ya kutolea elimu ili kuwafanya walimu watekeleze majukumu yao kwa ufasaha lakini pia kuwafanya wanafunzi wapokee kwa usahihi mafunzo yanayotolewa.

Upatikanaji wa nyumba mpya za kuishi watumishi kwenye shule za Sekondari Kikafu na Sawe kumesaidia kuwapatia walimu na watumishi wengine makazi ya uhakika na kusaidia kupunguza adha wanayopata watumishi wanapopanga kwenye nyumba za watu binafsi.

Shilingi milioni 300 zimetumika kuwapatia watumishi makazi ya uhakika katika shule hizo kwa kujenga nyumba zenye uwezo wa kutumiwa na familia sita kila moja na kufanya familia 12 kupata makazi.

Fedha za kufanikisha ujenzi wa nyumba

hizo zimetolewa na serikali kuu ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 inayolenga kuongeza idadi ya nyumba za kuishi walimu ili kuimarisha sekta ya elimu kwa shule za msingi na sekondari.

Kuwepo kwa makazi ya uhakika kwa walimu kumesaidia kwanza kuwaweka walimu karibu na mazingira ya shule na kupelekea walimu kutumia muda mwingi Zaidi kuwahudumia na kuwasaidia wanafunzi kwenye masomo na malezi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti; baadhi ya walimu wa

shule hizo wameonesha kui-shukuru Serikali kwa kujenga nyumba hizo ambazo kwao imewasaidia sana kuwajengea utulivu na kuwafanya watekeleze wajibu wao wa kufundisha wanafunzi kwa ufanisi zaidi. Pamoja na kupatikana nyumba hizo mbili zenye uwezo wa kukaliwa na familia sita kila moja bado halmashauri ya wilaya ya Hai inaendelea kutafuta uwezekano wa kujenga nyumba za namna hiyo kwenye shule zilizopo wilayani humo ili kupunguza na hatimaye kumaliza kabisa tatizo la nyumba za makazi ya walimu na kufanya walimu wote wakae karibu na shule wanazofundisha.

Shirika la Nyumba Lakamilisha Ujenzi Ofisi ya DC Hai

SHIRIKA la Nyumba nchini (NHC) limesema litaendelea kutekeleza miradi mbalimbali inayokabidhiwa na Serikali Kuu huku likizingatia viwango vinavyokubalika kitaalam.

Ahadi hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo Dkt. Maulid Banyani, wakati wa hafla ya kukabidhi jengo jipya la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, iliyofanyika wilayani humo.

“Tunaishukuru Serikali, hususan ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt. John Magufuli kwa kuendelea kuiamini NHC na kuipa miradi mbalimbali ambapo kwa sasa kuna miradi zaidi ya 40 ambayo inatekelezwa na NHC hapa nchini”, amesema.

Dkt. Banyani Amesema NHC kuendelea kuaminiwa na Serikali na kupewa miradi hiyo ni kazi nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa na shirika hilo wakati wa kutekeleza miradi mbalimbali ambapo alisema shirika hilo litaendelea kufanya kazi kwa weledi. .

Aidha amempongeza Rais Dkt. Magufuli kwa kuwa na maono yaliyopelekea Watanzania kuendelea kufanya kazi huku wakichukua tahadhari wakati Dunia ikiendelea kupambana na ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya Corona.

“Kama tungelazimishwa kujifungia ndani kama mojawapo ya tahadhari ya kuepusha maambukizi mapya ya virusi vya Corona



Jengo jipya la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai lililojengwa katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano

hata mradi huu usingeweza kukamilika kwa wakati uliowekwa na hapa ndipo umuhimu wa maono mazuri aliyokuwa nayo Rais wetu unaponekana”, Amesema Dkt. Banyani.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Yusuph Bigambo kutoka wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ambao walisanifu na kusimamia mradi huo kama Mshauri Elekezi Mkuu kwa ushirikiano na Mshauri Elekezi Msaidizi upande wa Umeme na Mitambo.

“Mradi huu ambao ume-tekelezwa na NHC kama Mkandarasi Mkuu ulianza rasmi Mei, 2019 na kukamilika Mei, 2020; mpaka sasa umegharimu jumla ya shilingi 1,092,327,322.92”, alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Dkt. Hatib Kazungu, Katibu Tawala Msaidizi Sekretarieti

ya Mkoa wa Kilimanjaro Bi Lydia Riwa amelipongeza Shirika la Nyumba kwa kukamilisha mradi huo kwa muda na ubora uliotarajiwa. “Nitoe rai kwa uongozi wa Serikali wilaya ya Hai kuhakikisha jengo hili linatunzwa vyema ili liweze kudumu kutokana na kuwa Serikali imetumia pesa nyingi katika kutekeleza mradi huu hii ikiwa ni sehemu ya ahadi ya Rais Dkt. Magufuli ya kuwepo na ofisi bora nchini kote”, alisema.

Akitoa shukrani kwa niaba ya uongozi wa wilaya ya Hai, Katibu Tawala wa wilaya hiyo Upendo Wela, amesihukuru Serikali kwa kutoa fedha zilizoweza ujenzi wa jengo ambapo amesema miundombinu bora hiyo itakuwa chachu ya viongozi wa Serikali ya wilaya hiyo kuongeza ufanisi wa utendaji wake hasa katika kuwahudumia wananchi.

DC Hai Alitaka Jeshi Kuzuia Uhalifu



Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya akizungumza na askari wa jeshi la akiba wilayani humo. Waliokaa kwenye viti ni Katibu Tawala Wilaya ya Hai Upendo Wella na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai Elia Machange

Mkuu wa wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro Lengai Ole Sabaya amelitaka Jeshi la akiba kwa kushirikiana na jeshi la polisi kuanza mara moja oparesheni za mara kwa mara zitakazo wezesha kujua maeneo yote yanayohusika na uzaji wa madawa ya kulevya pamoja na utengenezaji wa pombe haramu aina ya gongo ndani ya wilaya. Sabaya ametoa agizo hilo wakati wa kikao kazi na askari wa jeshi hilo la akiba katika viwanja vya Halmashauri hiyo ambapo amesema hivi sasa ni wajibu wao kuhakikisha wanafanya oparesheni hiyo ambayo pia itasaidia kujua,

kutambua wageni wote wanaoingia wilayani hapo na shughuli wanazozifanya kwa muongozo wa polisi kata lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa wilaya ya Hai inakuwa salama wakati wote. Pia amewatahadharisha kutokumuonea mtu yoyote wakati wa oparesheni hiyo huku akiwaasa kutokujiingiza katika biashara ya uzaji wa madawa ya kulevya pamoja na pombe haramu na kwamba atakayebainika kufanya hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria na kinidhamu. Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai Upendo Wella amewataka kuwa na uzalendo, nidha-

mu na kuzingatia kiapo walichoapa ili kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Naye kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Elia Machange amesema kuwa halmashauri iko tayari kushirikiana na jeshi hilo wakati wote huku akilipongeza kwani limekuwa na mchango mkubwa wa kulinda amani ndani ya wilaya.



Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya akizungumza na viongozi wa dini kuhusu masuala ya amani ya wilaya na Taifa.

Wilaya ya Hai Yajenga Kituo cha Afya kwa Mapato ya Ndani

Zaidi ya wanachi 27,000 wa kata za Weruweru, Mnadani na Masama Rundugai wanatarajia kunifuai na huduma ya afya kutoka katika kituo cha afya kinachojengwa katika kijiji cha Longoi kata ya Weruweru kinachokadiriwa kugharimu zaidi ya shilingi milioni 500 kutoka katika mapato ya ndani.

Akizungumza katika uzinduzi wa ujenzi wa kituo hicho uliofanyika katika Kijiji cha Longoi; Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya amesema ujenzi wa kituo hicho ni maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. John Magufuli kwenda kwa wasaidizi wake kuhakikisha wananchi wanasogezewa huduma muhimu kwenye maeneo yao.

Amesema fedha za awali za ujenzi wa kituo hicho kiasi cha shilingi 358,552,415, zimetokana na michango ya vyama vya ushirika wilayani humo na kwamba kukamilika kwa ujenzi huu utaupa heshima ushirika ambao kwa miaka

mingi sana umekuwa ukituhumiwa kwa ubadhilifu wa fedha.

“Milioni 358 itamaliwa za jengo la maabara ya upimaji, jengo la wagonjwa wa nje na jengo la mama na mtoto na akina mama waliokuwa wanatoka hapa wanavuka kale kadaraja ka reli usiku wa manane wanapitia Shirimgungani hadi Mijongweni hadi Shirimatunda hawatakwenda tena; huduma zenu sasa zimeletwa hapa” alisema Sabaya.

Awali akisoma taarifa ya ujenzi wa kituo hicho Mganga Mkuu wa Wilaya Dkt. Irene Haule amesema wazo la ujenzi wa kituo hicho cha Afya lilitolewa na mkuu huyo wa wilaya kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na Usalama na kwamba kitawasadia wananchi wa kata hizo ambao baadhi yao wamekuwa wakitembea umbali wa zaidi ya km 20 kufuata huduma za Afya katika



Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya akizindua ujenzi wa kituo cha afya kwa kuchimba msingi wa jengo.

hospitali ya Wilaya.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Yohana Sintoo ameahidi kuzisimamia kikamilifu fedha hizo na kuhakikisha kuwa ujenzi wa kituo hicho unakamilika kwa wakati huku akiwataka wananchi wa eneo hilo kutoiba wala kuharibu miundombinu ya mradi huo na kwamba yeyote atakaebainika atachukuliwa hatua za kisheria.

Nao baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Longoi; Mwajuma Athumani na Miraji Athumani wameishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kuwapelekea kituo hicho cha afya kwani wamekuwa wakitumia gharama kubwa kufuata

huduma za afya na wakati mwingine wamekuwa wakipoteza ndugu zao kutokana na huduma hizo kuwa mbali.

Wilaya ya Hai ina jumla ya vituo vya kutolea huduma 60 ambavyo kati ya hivyo vituo 2 Ni hospitali ya wilaya na hospitali teule ya Machame ambapo kati ya hivyo vimo vituo vya binafsi na vya mashirika ya dini.

Ujenzi wa kituo hicho cga afya unaendelea na hadi mwezi Ogasti 2020 jumla ya majengo matatu ya Maabara, Wagonjwa wa nje na jengo la mama na mtoto yamekamilika na yapo tayari kuanza kutoa huduma.

Watumishi 1000 Waajiriwa Kuimarisha Huduma Hai



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Yohana Sintoo akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo ikiwa ni sehemu ya kuimarisha utendaji wa kazi.



Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutengeneza mazingira ya kuwahudumia wananchi wake kwenye sekta mbalimbali zinazosimamiwa na serikali kuu, idara na taasisi za umma pamoja na mamlaka za serikali za mitaa. Halmashauri ya Wilaya ya Hai chini ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni moja ya wanufaika wa mipango ya serikali kuimarisha utoaji huduma bora kwa wananchi

hasa ikikumbukwa kwamba serikali za mitaa zinahudumia wananchi kwenye nyanja za elimu, afya, miundombinu na sekta nyingine hivyo kuwepo na aina tofauti ya watumishi wa sekta husika.

Ili kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi kwenye sekta zilizopo kwenye halmashauri ya wilaya ya Hai; serikali imefanya maboresho kadhaa ikiwemo kuongeza watumishi, kupandisha vyeo watumishi waliopo pamoja na kuongeza elimu ya watumishi.

Mwaka 2016/2017, serikali ilifanya zoezi la uhakiki wa watumishi katika kubaini uhalali wa kitaaluma wa watumishi husika ambapo jumla ya watumishi 61 walibainika kughushi na

kupoteza sifa za kuendelea na ajira walizokuwa wakizitumikia hivyo kuachishwa kazi.

Kwa sasa halmashauri hiyo ina watumishi 2,166 ambao wanafanya kazi katika idara 13 na vitengo 6 vinavyohudumia wananchi kwenye sekta zilizo chini ya mamlaka ya serikali za mitaa kukiwa na upungufu wa watumishi 906 katika sekta za elimu msingi, kilimo, mipango, afya, mifugo na walimu wa sayansi kwa shule za sekondari.

Serikali imeendelea kutafuta suluhisho la upungufu wa watumishi kwenye halmashauri kwa kuajiri watumishi wa kada mbalimbali ikiwemo kuajiriwa watu

Inaendelea. uk 19



Watumishi 1000 . . . Inatokauk 19

mishi wapya 103 wa kada za afya, walimu wa shule za msingi na sekondari, watumishi wa sekta za ardhi pamoja na watumishi wa kilimo, umwagiliaji na ushirika.

Aidha, serikali imewapandisha vyeo watumishi wa kada mbalimbali kwa zoezi maalumu ambapo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 watumishi 632 wamepandishwa vyeo kati yao walimu walikuwa 567 na 65 walikuwa mchangan-yiko wa watumishi wa kada nyingine huku zoezi jingine la kupandisha vyeo watumishi wa umma lilifanyika mwaka wa fedha 2017/2018 ambalo lilihusu watumishi 610 huku 401 wakiwa walimu na 209 kada nyingine.

Zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wa umma linakwenda sambamba na kuwabadilishia kiwango cha mshahara kulingana na utaratibu



wa mishahara ya watumishi wa umma kulingana na kada zao na vyeo vyao.

Katika kuimarisha utawala bora katika halmashauri ya wilaya ya Hai; serikali imeajiri afisa tarafa mmoja kuziba nafasi iliyokuwa wazi huku ikiajiri watendaji wa kata 8 wakiziba nafasi zilizokuwa wazi kwenye kata 17 za wilaya hiyo na watendaji 38 wa vijiji na kufanya vijiji vyote 62 kuwa na watendaji ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma kuanzia ngazi ya kijiji hadi halmashauri.

Uwepo wa mamlaka za serikali za mitaa ni utaratibu wa serikali kusogeza mamlaka kwenye maeneo ya karibu na wananchi ili kuimarisha utoaji huduma za elimu, afya, maji, upatikanaji na ukarabati wa miundombinu na huduma nyingine kwa ngazi ya wilaya, halmashauri, tarafa, kata na kijiji.



Mikopo ya Halmashauri Yainua Uchumi wa Wananchi



Katibu Tawala Wilaya ya Hai Upendo Wella na Mkurugenzi Mtendaji wakikabidhi hundi kwa kikundi kilichokidhi kupata mkopo wa halmashauri. Wanaoshuhudia ni Meneja wa benki ya NMB Hai Medard Malisa na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Lucas Msele

Serikali imeweka utaratibu wa kuwaendeleza wananchi wake kiuchumi kwa kutumia mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa na halmashauri. Halmashauri ya Wilaya ya Hai haipo nyuma kutekeleza mpango huo wa serikali kwa kutenga 10% ya makusanyo yake kutoa mikopo kwa wananchi wake waliojiunga kwenye vikundi ikiwemo vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Katika mgawanyo wa fedha hizo; asilimia 4% ni kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Wanawake; asilimia 4% ni kwa ajili ya kukopesha vikundi vya Vijana na asilimia 2% ni kwa ajili ya vikundi vya Watu Wenye Ulemavu. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri imetoa kiasi cha shilingi 109,973,528/= kwa ajili ya kuvikopesha Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo Mkopo uliotolewa kwa Vikundi vya Wanawake ni Tshs. 65,271,500/=, Vijana ni Tshs

35,702,028/= na Watu wenye Ulemavu ni 9,000,000/=.

Ikiwa ni juhudi za kuwafikia wananchi wengi iwezakavyo; jumla ya vikundi 27 vimepatiwa mkopo kati ya hivyo vikundi vya Wanawake ni 18, Vikundi vya Vijana ni 6 na vikundi vya Watu Wenye Ulemavu ni 3 vilivyonufaika na Mkopo huo wenye lengo la kuwainua wananchi kiuchumi.

Kwa kipindi cha Mwaka wa fedha 2019/2020 hadi mwezi Julai Halmashauri imetoa Jumla ya Tsh 179,602,904. Upatikanaji wa fedha hizo umesaidia wananchi wengi kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali ikiwemo kilimo na ufugaji kwa kuongeza mtaji, kuongeza maeneo ya kilimo pamoja na kufanya shughuli zao kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa sekta husika na hatimaye kuinua pato la kikundi na la mwanakikundi mmojammoja.

Moja ya kikundi kilichofaidika na mkopo wa halmashauri

ni Kikundi cha AGROP kinachojishughulisha na mradi wa kusindika mbogamboga na matunda. Kikundi hiki kimefanikiwa kupata mkopo wa shilingi 9,000,000 na kuanzisha miradi ya kuzalisha Wine ya Rozela, Banana Beverage, Tomato Sauce pamoja na kuzalisha Chilli Sauce. Aidha kikundi kina mipango ya kupata Bar code ili kuweza kupanua wigo wa kuuza bidhaa zake ndani na nje ya nchi; kupata eneo la kujenga kiwanda ili kuongeza uzalishaji lakini pia kutoa ajira kwa vijana wengi zaidi na kuchangia kwenye juhudi za serikali za kumaliza changamoto ya upungufu wa ajira kwa wananchi. Wakishuhudia mafanikio yaliyopatikana kupitia shughuli za kikundi cha AGROP baadhi ya wanakikundi wameishukuru serikali kwa maono chanya yaliyopelekea kufikiwa maamuzi ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ambayo kupitia hiyo wananchi wanafaidika na kuimarika kiuchumi.



Serikali Yafanya Maboresho Sekta ya Afya Wilayani Hai



Mwonekano wa ndani kwenye jengo jipya la wodi ya wanawake kwenye hospitali ya wilaya ya Hai

Halmashauri ya Wilaya ya Hai inaendelea kutoa huduma za afya kwa wananchi wake pamoja na wananchi wa maeneo jirani kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza katika ibara ya 50 (i) 64-76. Halmashauri imeweza kununua dawa za kiasi cha shilingi 2,681,637,491.95 na hivyo kufanya kiwango cha upatikanaji wa dawa kufikia asilimia 97 ukilinganisha na mwaka 2015 ambapo upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma ilikuwa ni asilimia 70, lengo kuu ni kuondoa kabisa tatizo la upatikanaji wa dawa katika vituo vya afya.

Ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya dawa saa 24 na kwa bei nafuu hasa kwa wanachama wa bima na wasio na bima; Halmashauri imetumia shilingi 41,485,900 kujenga duka la dawa kwa kutumia fedha zinazopatikana na huduma ya bima ya afya linalotoa huduma saa 24 kwa wananchi. Uwepo wa duka hili unawasaidia wananchi kupata dawa kwa wakati na kwa bei nafuu na imewapunguzia kwenda umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta huduma hiyo lakini pia duka hilo linatumika kama chanzo cha mapato kwa halmashauri hiyo. Kwa namna nyingine Serikali imekamalisha ujenzi wa wodi ya wanawake katika hospitali ya Wilaya ya Hai iliyogharimu kiasi cha shilingi 220,509,025; wodi ambayo kukami-

lika kwake kumeondoa adha ya wananchi wa Hai waliokuwa wanalazimika kupata huduma hiyo kwenye hospitali za wilaya ya jirani au hata Hospitali ya Mkoa. Aidha Wilaya ya Hai imeanzisha ujenzi wa kituo cha afya katika ukanda wa tanbarare kikiwa Sera ya uzazi salama imejikita katika kumlenga mama mjamzito kujifungua katika kituo cha kutolea huduma za Afya ili kuhakikisha usalama wake na wa mtoto. Tangu kuwepo kwa uhamasishaji na mafunzo ya uzazi salama kwa jamii kumekuwa na ongezeko kubwa la wajawazito kuhudhuria kliniki na pia kujifungua katika vituo vya kutolea huduma. Kumekuwa na ongezeko la wajawazito kwa asilimia 330% kwa mwaka 2020 ukilinganisha na asilimia 32.11% mwaka 2014. Pia kumekuwa na ongezeko la mahudhuro ya kliniki kwa wanaume ambao wamekuwa wakifika na kwa ajili

ya kupatiwa elimu juu ya uzazi wa mpango na kujizuia na maambukizi ya magonjwa ya zinaa. Hali hii ime-sababisha kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kutoka asimia 16% mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 4% mwaka 2018.

Kutokana na usimamizi madhubuti, wilaya ya Hai imeweza kufanya vizuri katika matukio mbalimbali ya kitaifa na mkoa ambapo kwa upande wa star rating (tuzo za nyota) wamefanikiwa kushika nafasi ya pili kimkoa hii ikiwa na maana ya kuboreka kwa huduma za afya katika Wilaya hiyo.

Wilaya ya Hai ni miongoni mwa Wilaya chache zenye kituo jumuishi kinachotumika kutoa huduma kwa wananchi hasa wale waliofanyiwa matukio ya ukatili wa kijinsia kinachofanya kazi kwa kushirikiana na Jeshi la polisi, daktari na ustawi wa jamii. Uwepo wa kituo hiki unasaidia kuwapunguzia wahanga wa matukio hayo usumbufu wa kuwafikia watoa huduma ambao kwenye kituo hiki wote wanapatikana kwenye eneo moja. Kwa mwaka 2015 hadi 2018 jumla ya kesi 22,368 zimeripotiwa na kushughulikiwa katika ofisi ustawi wa jamii na watoto 2,128 wameunganishwa na familia zao.

Katika kutekeleza sera ya kuwajali na kuwahudumia wazee, wilaya ya Hai imefanikiwa kuwafikia jumla ya wazee 4,199 waliopatiwa vitambulisho vinavyowasaidia kupata matibabu na zoezi linaendelea ili kuwafikia wazee wote wenye uhitaji.



Mwonekano wa jengo jipya la wodi ya wanawake kwenye hospitali ya wilaya ya Hai



Mwonekano wa jengo jipya la duka la dawa kwenye hospitali ya wilaya ya Hai

Wilaya ya Hai Yaimarisha Huduma za Kinywa na Meno

Serikali katika Wilaya ya Hai imeendelea kuimarisha huduma za afya kwa kujenga jengo jipya na kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kitengo cha kinywa na meno kwenye hospitali ya wilaya hiyo.

Akikagua maendeleo ya jengo hilo na vifaa vilivyounuliwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Yohana Sintoo amewataka wataalamu wa afya kwenye wilaya hiyo kutunza vifaa na miundombinu iliyopatikana kwa fedha za watanzania.

Aidha Sintoo amewataka wataalamu wa afya hususani wa kitengo cha afya ya kinywa na meno kutoa huduma bora kwa wananchi wote ili kuonesha thamani halisi ya uwekezaji unao-fanywa na serikali kwa lengo la kuhudumia wananchi wake.

Akizungumzia ujenzi wa jengo hilo; Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Hai Dkt. Ananoela Urassa amesema kuwa jengo hilo limejengwa kwa shilingi milioni 84 likiwa na vyumba vya mapokezi, kupumzikia, chumba cha daktari, sehemu ya mafaili ya wagonjwa na chumba kitakapowekwa kiti cha huduma za meno.

Amesema pamoja na jengo hilo; serikali imenunua kiti maalumu cha huduma za kinywa na meno kwa shilingi milioni 47 kitakachotumiwa kutolea huduma hizo.

Kwa upande wake Mratibu wa Kitengo cha Afya ya Kinywa na Meno Dkt. Faridu Kirita amei-



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Yohana Sintoo akikagua vifaa vilivyounuliwa kuboresha huduma za afya kwenye hospitali ya wilaya hiyo



pongeza serikali kwa kuwapatia jengo linalokidhi mahitaji ya kitengo hicho lakini pia kununua vifaa vya kisasa vya kutolea huduma.

Kirita amewahakikishia wananchi kupata huduma bora kwa kuzingatia uwepo wa wataalamu na vifaa husika kutoa huduma za afya ya kinywa na meno huku akibainisha kuwa vifaa vilivyounuliwa ni vya kisasa ikiwemo kiti kinachoweza kutolea zaidi ya huduma kumi kulingana na mahitaji au matatizo ali-yonayo mgonjwa.

Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuimarisha utoaji huduma za afya kwenye wilaya ya Hai kwa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora za afya ikiwemo kujenga wodi kwenye hospitali ya wilaya, kujenga duka la dawa, kununua dawa na vifaa tiba kwa matumizi ya hospitali na vituo vingine vya kutolea huduma.

Katika kuongeza miundombinu ya afya serikali inajenga kituo cha afya kwenye kata ya Weruweru pamoja na ujenzi wa zahani kwenye vijiji kadhaa vya wilaya ya Hai.



Wilaya ya Hai Yanufaika Maboresho Elimu Msingi



Mwalimu na Wanafunzi wa Shule ya Msingi Gezaulole wakifurahia moja ya madarasa yaliyojengwa katika mpango wa kuboresha elimu.

Wilaya ya Hai ni moja ya wilaya zinazofaidika na mpango wa serikali kuimarisha sekta ya elimu ambapo pamoja na shughuli nyingine zinazoendelezwa na serikali kama kuimarisha miundombinu, kuajiri walimu na kufanikisha upatikanaji wa vitabu na vifaa serikali inafanikisha wanafunzi wote kupata elimu bila malipo.

Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 serikali imetoa kiasi cha shilingi 2,465,942,651.46 kwa ajili ya kugharamia elimu bila malipo. Hatua hii ya kufanya elimu itolewe bila malipo imefanya kuwepo kwa ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa kwa ajili ya elimu msingi kutoka 4,201 mwaka 2015 hadi kufikia 4,474 mwaka 2020 amba-

po kwa darasa la awali wameongezeka kutoka wanafunzi 3,843 mwaka 2015 hadi kufikia 4,160 mwaka 2020.

Kitendo cha kutoa elimu bila malipo kimepelekea watoto ambao wazazi wao hawakuwa na uwezo wa kuwalipia ada kupata nafasi ya kuandikishwa shuleni. Katika kuendana na ongezeko la wanafunzi; uhamasishaji umefanywa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji na kufanikiwa kujenga vyumba 35 vya madarasa, matundu 120 ya vyoo.

Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ufuatiliaji wa shule ambapo kwa mwaka 2018 serikali ilitoa pik-

ipiki 17 kwa ajili wa waratibu elimu kata waliopo katika wilaya ya Hai kwa ajili ya kusaidia kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa shule na hivyo kusababisha kuwa na matokeo mazuri ambapo kwa matokeo ya mwaka 2019 Wilaya ya Hai ilishika nafasi ya pili kimkoa na nafasi ya 20 kitaifa huku hali ya ufaulu wa mitihani wa darasa la saba ukiongezeka kutoka 91.24% mwaka 2015 hadi 92.8% mwaka 2019.

Halmashauri inaendelea kuboresha miundombinu ya shule kwa kukarabati na kujenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vyoo safi na salama pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote kwa kutumia mapato ya ndani. Hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Hai inazo shule za Msingi 128 zikiwemo za Serikali 105 na shule za binafsi 23 ambapo idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ni 35,282 huku kukiwa na wavulana 17,929 na wasichana 17,353 wakati shule za binafsi zina wanafunzi 5,565 kati yao wavulana 2,830 na wasichana 2,735.



EP4R Yasaidia Kupunguza Msongamano Darasani Shule ya Msingi



Moja ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa na serikali kupitia Utaratibu wa EP4R kwenye Shule ya Msingi Chekereni

Baada ya serikali ya awamu ya tano kutangaza elimu kutolewa bila ada kwa wanafunzi na kuhamasisha wazazi kuandikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule kuhakikisha kuwa wanaandikishwa imepelekea kuongeza idadi ya wanafunzi na kwa upande mwingine kuibua changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Serikali imefanikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule mbalimbali za msingi katika wilaya ya Hai ikiwemo Shule ya Msingi Chekereni iliyopo kata ya Masama Rundugai.

Wanafunzi katika shule hii ya Msingi walikuwa

wakisongamana darasani ambapo kwa mwaka 2015 jumla ya wanafunzi 157 walikuwa wanatumia chumba kimoja cha darasa.

Ujenzi wa vyumba vya madarasa kupitia mradi huu umesaidia kupunguza idadi ya wanafunzi na kwa mwaka 2020 wanafunzi wanaotumia chumba kimoja cha darasa ni 45 tu na wanapata nafasi ya kujifunza vizuri kwa nafasi.

Mradi huu uliofadhiliwa kwa ruzuku ya serikali kupitia mpango wa EP4R umegharimu Shilingi 25,000,000/= kwa kumaliza ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa ambavyo maboma yamejengwa hadi ki-

wango cha lenta kwa nguvu ya wananchi na fedha hizo zimetumika kufanya umaliziaji.

Kazi zilizofanywa kwenye mradi huo ni pamoja na kupaua, kupanga mawe, kuweka sakafu, kupiga plasta, kuweka milango na madirisha pamoja na kuweka samani ikiwemo madawati, meza na viti vya mwalimu.

Ukamilishwaji wa mradi huu umeinua kwa kiasi kikubwa ari ya wanafunzi kupenda kusoma kwani wanapata nafasi ya kwenye madarasa lakini pia imesaidia kuwapatia nafasi watoto wote wenye umri wa kwenda shule na hatimaye kuongeza ufaulu kwenye mitihani.

Elimu Sekondari Yapewa Umuhimu Wilayani Hai

Elimu ya sekondari ni hatua muhimu kwenye maendeleo ya mwanadamu katika nyanja ya kielimu kwani ni hatua ya pili ya makuzi ya mwanafunzi baada ya kuhitimu mafunzo ya darasa la saba ikiwa ni ngazi ya elimu ambapo mwanafunzi anaanza kutengenezewa msingi wa eneo la kuboea baada ya mafunzo hasa afikapo kidato cha tatu anapochagua mchepuo wa kusoma ikiwa ni sayansi, Sanaa au biashara.

Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa sasa ina shule 46 za sekondari kati ya hizo 30 ni za serikali na 16 ni za binafsi na taasisi za kidini. Katika shule za serikali kuna jumla ya wanafunzi 12,740 ikiwa wavulana ni 6,244 na wasichana 6,496 huku shule za serikali zikiwa na walimu 567.

Kwenye sekta ya elimu hususani upande wa elimu sekondari, kwenye halmashauri hii Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 imetekelezwa kwa namna mbalimbali ikiwemo mapokezi ya kiasi cha shilingi 3,427,170,065.50 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwenye shule za sekondari na shilingi 5,926,461,980.19 kute-



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Yohana Sintoo akiwa na baadhi ya wanafunzi waliofanya vizuri mitihani aliowaalika ofisini kwake kuwazawadia.



keleza elimu bila malipo ili kuwawezesha wanafunzi wote waweze kupata elimu bila ubaguzi.

Pamoja na fedha za kuhudumia elimu bure, serikali imeendelea kuongeza nyumba za walimu kutoka 97 mwaka 2015 hadi 99 mwaka 2020 kwa kujenga nyumba mbili zenye uwezo wa kutumiwa na familia sita kila



moja (six-in-one).

Kuongeza vyumba vya mada-rasa kutoka vyumba 308 hadi vyumba 316 pamoja na kuongeza matundu ya vyoo kutoka 456 mwaka 2015 hadi 460 mwaka 2018 na kuongeza maabara kutoka 6 hadi 25.

Mipango mbalimbali inayofanyika kuimarisha upatikanaji na hali ya utoaji elimu imesaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi kwenye mitihani ya kitaifa ambapo ufaulu wa kidato cha kwa mwaka 2019 umeongezeka na kufikia asilimia 86 na kushika nafasi ya 7 kimkoa huku matokeo ya kidato cha nne kuongezeka kutoka asilimia 61% mwaka 2015 hadi 81% mwaka 2019 na ufaulu wa kidato cha sita kuendelea kuimarika kutoka 99.71% mwaka 2015 hadi 99.91% mwaka 2020 ikiwa ni pamoja na kufanikiwa kutoa mwanafunzi mmoja kwenye nafasi kumi bora za kitaifa.



Ujenzi wa Ukuta Waimarisha Usalama Sekondari ya Wasichana Machame

Shule ya sekondari ya Wasichana Machame ni shule ya serikali iliyoanzishwa mwaka 1947 ikiwa kama shule ya wamisionari katika wilaya ya Hai, mkoani Kili-manjaro.

Shule hii ina utajiri wa watu mashuhuri waliowahi kusoma shuleni hapo akiwemo Bi. Sifaeli Shuma ambaye ni shujaa wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na ndiye aliyebeba kibuyu cha udongo wa Tanganyika na kumkabidhi Hayati Mwalimu J.K Nyerere kabla ya kuuchanganya na udongo wa Zanzibar; pia yupo aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi Bi. Ritha Mlaki.

Ujenzi wa uzio kuzunguka maeneo ya shule hiyo ni moja ya hatua za muhimu zinazochukuliwa na serikali kuimarisha shughuli za ufundishaji na kujifunza kwenye shule hiyo huku lengo kuu likiwa kuinua ufaulu wa wanafunzi.

Uwepo wa uzio huo unasaidia kuweka shule kwenye mazingira salama zaidi huku ikihakikisha usalama wa walimu, wanafunzi na mali zao hivyo kusaidia wanajamii wa shule hiyo kutekeleza wajibu wao wa msingi wa kufundisha na kujifunza bila kuhofia usalama wao binafsi na mali zao.

Uzio wenye urefu wa mita 1,068 umejengwa kwa kutumia matofali huku sehemu ya uzio wenye urefu wa mita 460 umejengwa kwa kutumia waya ikiwa ni juhudi za makusudi za serikali kuimarisha usalama kwenye viunga vya shule hiyo.

Uzio uliogharimu kiasi cha shilingi 160,645,520 umesaidia pamoja na mambo mengine; kuimarisha afya za wanafunzi kwani uzio huo umesaidia juhudi za kudhibiti aina ya vyakula wanavyokula wanafunzi hasa vile vinavyopikwa mitaani na kuuzwa kinyemela

kwa wanafunzi bila kuzingatia kanuni za afya.

Kupungua kwa utoro wa wanafunzi ni moja ya mafanikio yaliyopatikana kwa kujengwa kwa uzio huo kwa kuzingatia umuhimu wa nidhamu kwenye safari ya kutafuta elimu.

Uwepo wa uzio umesaidia kuziba njia zisizo rasmi zilizokuwa zinatumiwa na wanafunzi kutoroka eneo la shule na kuwasababisha kukosa baadhi ya vipindi vya masomo.

Shule ya sekondari ya wasichana Machame ikiwa moja ya shule kongwe nchini imjiwekea mikakati ya kufanya vizuri kwenye mitihani ya ndani ya mkoa na ile ya Taifa kwa kuimarisha shughuli za kujifunza na kufundisha wanafunzi kwa kuzingatia mtaala wa elimu lakini pia kutoa malezi bora kwa wanafunzi wote.



Bweni Lachangia Kuanzishwa Kidato cha Tano



Mwonekano wa Bweni la wanafunzi kwenye Shule ya Sekondari Harambee

Ujenzi wa bweni hili umafanyika ili kuongeza wigo wa shule zenye kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Baada ya serikali kuanza kutoa elimu bila ada kwenye ngazi ya elimu ya msingi na sekondari hadi kidato cha nne kumetokea ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano.

Sambamba na kutoa elimu bure; serikali pia imeimarisha kazi nzima ya kutoa elimu kwa kua-jiri walimu, kuboresha miundombinu na kufanikisha upatikanaji wa vitabu na mahitaji mengine ya vifaa vya kujifunzia.

Kuimarika kwa sekta ya afya hususani ujenzi wa zahanati kwenye vijiji, vituo vya afya kwenye kata pamoja na upatikanaji mzuri wa dawa umepelekea wanafunzi kutumia vizuri muda wa masomo na hivyo kuinua kiwango cha ufaulu.



Hapo ndipo kulipotokea uhitaji wa shule zenye kidato cha tano na cha sita ili kuwapokea wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kufaulu vizuri kuingia kidato cha tano.

Ujenzi wa bweni kwenye shule ya sekondari Harambee umesaidia kuanzisha elimu ya kidato cha tano kwa ajili ya wanafunzi wasichana na shule hiyo imesajiliwa kwa wanafunzi

wanaosoma mchepuo wa Sanaa huku maandalizi yakiendelea kuiongezea sifa ikiwemo ujenzi wa maabara ili iweze pia kupata usajili wa mchepuo wa sayansi.

Bweni hilo la ghorofa moja lenye uwezo wa kupokea wanafunzi 120 limejengwa kwa gharama ya Shilingi 203,086,000 ikiwa ni ushirikishwaji kati ya serikali kuu, halmashauri ya wilaya ya Hai, wananchi pamoja na wadau mbalimbali.

Ujenzi wa Maabara Kuimarisha Elimu



Maabara kwenye Shule ya Sekondari Harambee

Baada ya kukamilika ujenzi wa bweni kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na kuanza masomo kwa michepuo ya Sanaa; mipango ya kuongezea michepuo ya sayansi ikaendelea kukamilishwa kwa kuanzisha ujenzi wa maabara zitakazotumiwa na wanafunzi kwenye kujifunzia masomo ya sayansi.

Lengo kuu la mradi huu wa ujenzi wa maabara ni kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo masomo wanayofundishwa kwa nadharia ili kuimarisha uelewa wao.

Ujenzi huo umehusisha vyumba vitatu vya maabara, uwekaji wa mfumo wa gesi kwa ajili ya matumizi wakati wa masomo, kuweka mfumo wa umeme pamoja na mifumo wa maji na shimo la maji

taka.

Vyumba vya maabara vilivyojengwa kwa thamani ya Shilingi milioni 48,257,850 vimekamilika na kwa sasa vinatumiwa



Maabara kwenye Shule ya Sekondari Tambarare

HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI			
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI WA CHAMA CHA MAPINDUZI			
2015 KWA KIPINDI CHA JANUARI 2016 - JUNI 2020			
IDARA/SEKTA	MRADI/SHUGHULI	MAHALI ULIPO	KIASI KILICHOTOLEWA
ELIMU MSINGI	Umaliziaji wa chumba cha darasa Shule ya msingi Nkwasinge	Machame Uroki	20,000,000
	Umaliziaji wa chumba cha darasa Shule ya msingi Orori	Narumu	20,000,000
	Ujenzi na umaliziaji wa chumba cha darasa Shule ya msingi Gezaulole	Bomang'ombe	35,500,000
	Umaliziaji wa chumba cha darasa Shule ya msingi Hai	Bomang'ombe	20,000,000
	Ujenzi na maliziaji wa vyumba vya madaras aShule ya msingi Bomani	Bomang'ombe	60,000,000
	Umaliziaji wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Bondeni	Masama Magharibi	40,000,000
	Umaliziaji wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Chekereni	Masama Rundugai	25,000,000
	Umaliziaji wa nyumba ya mwalimu Shule ya msingi Chekereni	Masama Rundugai	25,925,000
ELIMU MSINGI	Umaliziaji wa nyumba ya mwalimu Shule ya msingi Njoro	Mnadani	28,500,000
	Ukarabati wa Choo cha wanafunz iShule ya msingi Kambi ya Raha	Muongano	1,000,000
	Ujenzi wa Choo cha walimu Shule ya msingi mijongweni	Mnadani	7,000,000
	Ujenzi wa choo cha wanafunzi Shule ya msingi Kyuu	Masama Magharibi	12,000,000
	Ujenzi wa Jiko la kupikia chakula cha wanafunzi Shule ya msingi Kyeeri	Machame Magharibi	3,450,000
	Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Mkalama	Masama Rundugai	23,400,000
	Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Uhuru	Bomang'ombe	38,043,000

	Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Msumadi	Masama Kusini	75,000,000
	Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Mlima shabaha	Mumungano	22,900,000
	Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Kengeroka	Bondeni	14,500,000
	Ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya msingi Masama Temu	Masama Mashariki	16,169,000
	Ujenzi wa choo cha wanafunzi Shule ya msingi Miaseni	Masama Mashariki	6,900,000
	Ujenzi wa madarasa 4 na matundu 5 ya choo shule ya msingi Kibaoni	Bomang'ombe	87,500,000
		JUMLA	495,287,000
ELIMU SEKONDARI	Ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Sekondari Kyuu	Masama Magharibi	70,000,000
	Ujenzi wa nyumba ya walimu 6 (Six in one) na vyumba 4 vya madarasa katika Shule ya sekondari Kikafu)	Machame Magharibi	150,000,000.00
	Ujenzi wa uzio wa tofali mita 1,068 na uzio wa waya mita 460 katika shule ya sekondari ya wasichama Machame	Machame Kaskazini	160,645,520.00
	Ujenzi wa bwani la Wasichama shule ya sekondari Harambee	Machame Kaskazini	200,386,000.00
	Ukamilishaji wa maabara 3 katika shule ya sekondari Harambee	Machame Kaskazini	48,257,850.00
	Ujenzi wa jengo la utawala katika shule ya sekondari Nkwamasi	Machame Kaskazini	158,926,194.50
	Ujenzi wa maabara 1 katika shule ya sekondari Tambarare	KIA	33,602,000
	Ujenzi wa madarasa 2 Shule ya Sekondari KIA	KIA	50,000,000
	Ukamilishaji wa maabara 2 shule ya sekondari Longoi	Weruwereu	10,000,000.00

	Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 4 ya vyoo shule ya sekondari Longoi	Weruweru	66,400,000.00
	Ukamilishaji wa chumba 1 cha darasa ya shule ya sekondari Longoi	Weruweru	12,600,000.00
	Ukamilishaji wa maabara 1 shule ya sekondari Rundugai	Masama Rundugai	10,000,000.00
	Ujenzi wa darasa 1 shule ya sekondari Lerai	Bondeni	20,000,000.00
	Matengenezo ya meza na viti shule ya sekondari Hai day	Bomang'ombe	5,901,032.00
	Ukarabati wa shule Kongwe - Shule ya Sekondari Lyamungo	Machame Mashariki	799,443,156
	Ukarabati wa shule Kongwe - Shule ya Sekondari Machame	Machame Kaskazini	976,115,828
		JUMLA	1,796,161,753
AFYA	Ujenzi wa jengo la kupumzishia wagonjwa katika zahanati ya Kia	kata ya Kia	99,966,888
	ujenzi wa kichomea taka katika Hospitali ya Wilaya	kata ya Bomang'ombe	5,000,000
	ujenzi wa kituo cha afya Longoi	kata ya weruweru	358,552,415
	Ukamilishaji wa jengo la zahanati ya kwatitu	kata ya Mmadani	30,000,000
	ujenzi wa jengo la kinywa na meno katika Hospitali ya Wilaya	kata ya Bomang'ombe	52,000,000
		JUMLA	545,519,303
MAENDELEO YA JAMII	Kuhakikisha kwamba Halmashauri inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya	Kata zote 17	338,836,404
MAENDELEO YA JAMII	Kuhakikisha Halmashauri inanzisha vituo maalumu ili kuwawezesha Vijana kupata sehemu ya kujifunza kwa vitendo shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kupata raarifa mbalimbali za maendeleo.	Kata ya Mmadani kijiji cha Shiri njoro	
MAENDELEO YA JAMII	Kuwawezesha vijana 200 ili waweze kujijari katika kazi za mikono, kilimo, ufundi na michezo.	Kata mbalimbali	
		JUMLA	338,836,404

KILIMO	Ujenzi wa jengo/kiwanda cha kusindika zao la vanilla kwa umoja wa wakulima wanachama zao la vanilla mkoa wa Kilimanjaro (UWAVAKI)..	Mwadani	168,782,403
	Ukarabati wa skima 3 za ununuzi katika mifereji ya Nsanya, Mosa Mwanjanga na Kikara Chini.	Narvon, Mmadani na Weruweru	844,000,000
	Ujenzi wa kituo cha Rasilimali za kilimo	Masama Rindogai	131,600,000.00
	Ujenzi wa kituo cha Rasilimali za kilimo	Mmadani	98,000,000.00
		JUMLA	1,242,382,403
MAII	Upauzi wa skima ya Losoa - KIA	KIA, Masama Kusini na Masama Rindogai	2,764,314,975.00
	Ukarabati wa skima ya Lyanungo - Umbwe	Narvon, Masama Kusini, Mmadani, Machame Mashaniki na Weruweru	65,399,435.00
	Mradi wa 'Lipa kwa Matokeo' (Payment by Results)	Masama Kusini, Banzang'ombe	515,075,227.44
		JUMLA	3,344,789,637.44





Limeandaliwa na:

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Hai
S. L. P. 27
Hai - Kilimanjaro
email: ded@haidc.go.tz
Blogu: www.wilayayahai.blogspot.com
Tovuti: www.haidc.go.tz





Wilaya ya Hai



2020

January						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

February						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
						1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

March						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30	31				

April						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30		

May						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30
31						

June						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30				

July						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

August						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
						1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29
30	31					

September						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30			

October						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

November						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30					

December						
Sun	Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30	31		